

Hatimaye kilio chetu kimesikia!


***Na: Jacqueline Tesha - Mratibu wa
Kanda ya Kaskazini***

Mradi wa Haki katika Misitu Tanzania ambao unamalengo ya kuhimiza uboreshwaji wa utawala na kuongezeka kwa uwajibikaji katika sekta ya misitu. Mradi kwa kupitia mikakati yake ya ufuatiliaji wa utawala wa misitu na hali ya misitu pamoja na tafti, chambuzi na mawasiliano, umeanza kuleta mafanikio makubwa sana hasa kwa wananchi wanaoishi katika tarafa ya Amani wilayani Muheza mkoani Tanga.

Mafanikio haya yametokana na makala iliyoandikwa na waandishi wa habari ambao walitembelea msitu wa Derema mwaka jana mwezi wa saba. Katika mkala hiyo ambayo ilirushwa na kituo cha ITV pamoja kutolewa na gazeti la kiingereza la "the guardian" wananchi waliomba serekali kuishirikisha katika kusimamia msitu wa Derema ambao ulikuwa umeharibiwa na watu wasiokuwa na nia njema kwa uvunaji haramu wa mbao. Wananchi hao walisema wakiacha msitu huo kuharibiwa wao



***Mama Bertha Anderson akielezea kuhusu
ushirikiano ambao wameanza kuupata toka
serikalini katika kuuhifadhi msitu wa Derema***



ndio watapata adhari za uharibifu wa msitu huo kwa kuwa wanategemea msitu huo kwa chazo cha maji na zaidi kwa ufugaji wa vipepeo ambavyo huviuza nchini Uingereza na Marekani na hivyo kujipatia fedha za kuendeshea maisha yao ya kila siku.


Manukato ya maombi hayo yalianza kunukia pale ambapo maafisa toka wilayani walipofika katika maeneo hayo na kuanza kutoa mafunzo kwa wananchi na kisha kuwashirikisha katika kufanya tathmini ya rasilimali za msitu huo wa Derema. Shughuli hiyo ilihusisha Maafisa Msitu wa Hifadhi wa Wilaya, Serikali za Vijiji na wajumbe 10 toka katika kila kijiji cha Kambai, Kwezitu, Kisiwani, IBC Msasa na Kwemdimu. Hatua hizo zilizofanyika ni za awali tu, katika mchakato mzima wa kuwashirikisha wanajamii katika kuulinda na kuusimamia msitu huo wa Derema.

Akizungumzia tukio hilo mjumbe wa Bodi ya MJUMITA kanda ya Kaskazini, Mama Bertha Anderson alisema kua wamefurahishwa sana na hatua hiyo ya serikali kwa kuwa kilikua ni kilio chao cha muda mrefu sana na hatimaye wameanza kuona matokeo yake. Alisema pia mchakato huo bado utaendelea hadi hapo wananchi watakaposhirikishwa kikamilifu katika usimamizi wa rasilimali hiyo. Aliongezea kuwa kama kitendo hicho kitafanikiwa, itasaidia sana katika kupunguza uharibifu katika msitu huo maana vijiji vinavyozunguka msitu huo vyote vitakuwa vimehusishwa katika ulinzi, pia alisema hii itauwezesha msitu kurudi katika hali yake ya nzuri ya awali na kuiwezesha jamii ya sasa na ya baadae kunufaika na rasilimali za msitu kutokana na usimamizi huo endelevu utakaokua ukifanyika.

Akitoa ufafanuzi wa kina juu ya suala hilo Afisa Misitu

Ya Hifadhi wa wilaya ya Muheza, Ndugu Rashidi alisema kuwa ni kweli zoezi hilo litaendelea na kuhakikisha jamii inashiriki katika Usimamizi wa pamoja wa msitu huo. Pia alitoa shukrani nyingi kwa MJUMITA na TFCG kupitia makala iliyofanyika katika eneo hilo kwa sababu imeleta muamko mkubwa kwa wananchi na serikali kwa sababu baada ya makala hiyo wamepatiwa fedha na idara ya misitu na nyuki kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo. Aidha, Ndugu Rashid alizungumzia kuhusu changamoto ambayo hadi sasa bado haijapatiwa ufumbuzi kuwa ni wananchi walioahidiwa kuachia ardhi ambayo walikuwa wanalima ndani ya msitu huo ili wapatiwe mashamba katika shamba moja la mkonge wilayani hapo, ahadi ambayo mpaka hivi sasa haijatekelezwa na hivyo wananchi wengi kuhoji kila mara kuhusu utekelezaji wa ahadi hiyo. Alisema wao hawana namna ya kufanya kuhusu ahadi hiyo na kuwa jambo hilo liko katika ngazi ya kitaifa.

MJUMITA inaisihi serekali kutimiza ahadi yake kwa wananchi ili wakati msitu huo ukirudi katika hali yake nzuri ya awali kwa kasi baada ya wananchi hao kuacha kulima ndani ya msitu huo basi maisha ya wananchi hayo pia yanawiri kwa kuwa na maeneo mbada ya kilimo kama walivyoahidiwa na serekali.



“UKIMWI

upo na unaua, mpaka sasa hakuna tiba wala kinga..
Ukimwi umeendelea kuwa adui wa nguvu kazi ambazo zingetumika katika uhifadhi wa misitu yetu. Hakuna namna tunaweza kutenganisha uhifadhi wa misitu yetu vizuri na afya zetu. Tuchukue tahadhari kwa kukwepa njia zote zinazoweza kutusababishia maambukizi ya ugonjwa huu hatari”

